

Utetezi wa Hali ya Hewa kwa Tanzania – Mtazamo Endelevu wa Mabadiliko ya Hali ya Hewa

**Mwaliko wa mazungumzo ya wazi ya mtandaoni siku ya Alhamisi, Januari 13, 2022
saa 10 hadi 12 jioni (saa za Ujerumani), saa 12 jioni hadi saa 2 usiku (saa za Tanzania)**



Malya Farm, East of Lake Victoria Diozese, Tanzania. Foto: K. Davis

Mabadiliko ya hali ya hewa yapo kila mahali. Athari za mabadiliko ya hali ya hewa msimu uliopita wa kiangazi zilionekana nchini Ujerumani na kote Ulaya kutokana na mafuriko, mioto ya porini pamoja na halijoto ya joto zaidi kuwahi kurekodiwa. Washirika wetu nchini Tanzania tayari walikumbana na athari hizo na nyinginezo za ongezeko la joto duniani kwa muda mrefu zaidi. Mabadiliko ya hali ya hewa ni janga la kimataifa na yanahitaji hatua za pamoja na madhubuti pia kwa upande wa makanisa. Kuna masuluhisho mengi na miradi ya kutia moyo ambayo tayari imetekelezwa.

Kwa majadiliano haya ya mtandaoni tunataka kuangazia jukumu la makanisa na mtazamo wa kitheolojia wa kujitolea kwa utetezi wa hali ya hewa na hatua za kuchukua kuhusu hali ya hewa. Zaidi ya hayo tutakuwa na mtazamo wa pamoja juu ya ukweli na takwimu kuhusu migogoro ya hali ya hewa na athari zake kwa Tanzania. Zaidi ya hayo tunataka kupata msukumo wa mradi bora wa utendaji „Maji kwa ajili ya Malya“ na kujadili kile kinachohitajika ili kuchukua hatua pamoja na kuanzisha miradi zaidi na mabadiliko katika makanisa yetu.

Tunataka kujadili kuhusu mada zifuatazo:

Mabadiliko ya Hali ya Hewa na Utetezi wa Hali ya Hewa - Misingi Yetu ya Kitheolojia

Askofu Andrew Gulle, Dayosisi Mashariki ya Ziwa Victoria (DMZV)

Askofu Tilman Jeremias, Jimbo la Kanisa la Mecklenburg na Pomerania

Utetezi wa Hali ya Hewa: Takwimu, Ukweli na Mahusiano

Uli Eder, Dawati la Taarifa za Utetezi wa Hali ya Hewa, Kituo cha Huduma za Kimataifa na Mahusiano ya Kiumoja (ZMÖ)

Athari za Mabadiliko ya Hali ya Hewa Tanzania

Paul Mpazi, Mkuu wa Idara ya Mipango na Uwekezaji, DMZV

„Maji kwa ajili ya Malya“ - Njia Endelevu ya Mabadiliko ya Hali ya Hewa

Joygrace Shoo, Mratibu wa Maendeleo ya Miradi, DMZV

Anne-Christina Achterberg, Mratibu wa Maendeleo ya Miradi, DMZV

Muongozaji:

Judith Meyer Kahrs, Dawati la Taarifa za Utetezi wa Hali ya Hewa na

Katharina Davis, Mratibu wa Dawati la Afrika, Kituo cha Huduma za Kimataifa na Mahusiano ya Kiumoja.

Usajili na Tafsihi: Ili kushiriki katika mazungumzo yetu ya mtandaoni bila malipo, jisajili sasa kupitia kiungo kifuatacho:

<https://zoom.us/meeting/register/tJMuc-2uqzoqHtBi1p0JYj3vjH5gPzoMd2IE>

Chumba cha mkutano wa mtandaoni kitafunguliwa dakika 30 kabla ya tukio kuanza. Tukio litafanyika kwa Kiingereza. Kutakuwa na tafsihi ya Kijerumani na Kiswahili ya michango itakayotolewa.

Tukio hilo limeandaliwa na Kituo cha Huduma za Kimataifa na Mahusiano ya Kiumoja cha Kanisa la Kiinjili la Kilutheri la Kaskazini mwa Ujerumani kwa ushirikiano na Dayosisi Mashariki ya Ziwa Victoria na Ofisi ya Kiumoja ya Jimbo la Kanisa la Mecklenburg.

mehr Informationen unter: nordkirche-weltweit.de



**ZENTRUM FÜR
MISSION UND ÖKUMENE**
Nordkirche weltweit